© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Sifa zote njema ni zenye kumthubutukia Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah), ambae Milki ya Mbingu na Ardhi iko kwenye Mkono Wake. Na Ufalme ni wake Yeye, na Sifa zote njema. Nae ni mwenye kushuhudia kila kitu. Maamrisho yote yatokayo Kwake na Qadar yametokamana na Hikma Zake. Anafanya atakavyo na kuamuru atakavyo. Nashuhudia yakwamba hapana anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake, asie na mshirika, Alie mlinzi, na Anaestahiki kusifiwa kwa kila Sifa njema. Nashuhudia yakwamba Muhammad ni mtumwa wake na mjumbe, ambae ni Mtume wa mwisho na ni kiongozi wao, na mbora wa wenye kuabudu; Tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah) amtukuze na azifikilize Amani kwa ukamilifu juu ya ahli zake, maswahaba zake na wote wenye kuandama uongofu wake kwa wema hadi siku ya malipo.

Kwanza kabisa...

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wa ta'aalah), katika kutufahamisha kuhusu Uwezo Wake usio na kifani na Hikma zenye ukamilifu, yakwamba yale anayo-yaamrisha Yeye Peke Yake ndiyo yanayo-tokea, na kwamba Yeye ndie anaewamiliki na kuwatawala watumwa Wake na kuwalinda, na kuwakhofisha, na kuwasahilishia, na kuwafanyia uzito, na kuwafanyia wepesi, kuwafanyia dhiki, na kuwanyoshea mambo yao, na kuyafanya mambo yao kufaulu. Akasema Mwenyezi Mungu (kama ilivyo fasiriwa):

يَسْـَٔلُهُۥ مَن فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۚ كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِى شَأْنٍ ﴿٢٩﴾

"Vinamuomba Yeye kila vilivyomo mbinguni na ardhini: kila siku Yeye yumo katika mambo (kama vile kuwatukuza wengine, kuwadhalilisha wengine, kuwahuisha wengine, kuwafisha wengine n.k)!" [Soorah ar-Rahmaan 55:29]

Kwahivyo Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) ndie anae-endesha mambo ya viumbe vyake kwa kuwalazimisha juu ya sheria Zake kulingana na Hikma Zake na Rehma Zake, na wakati mwengine kulingana na Hikma zake na Uadilifu, na wala Mola wako hamdhulumu yeyote; maelezo hayo yamo kwenye Qur'aani (kama ilivyo fasiriwa):

وَمَا ظَلَمْنَـٰهُمْ وَلَـٰكِن كَانُوا۟ هُمُ ٱلظَّـٰلِمِينَ ﴿٧٦﴾

"Wala Sisi hatukuwadhulumu, bali wao wenyewe walikuwa madhalimu (wa nafsi zao)." [Soorah az-Zukhruf 43:76]

Enyi Waislamu:
Kwa yakini sisi tunamuamini Mwenyezi Mungu na Qadar Yake, na kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu ni miongoni mwa nguzo za Imaan [1]. Tunaamini yakwamba kila jambo zuri au hali ya utulivu na usalama tulionao, basi hayo yametokamana na Baraka za Mwenyezi Mungu juu yetu na tunawajibika sisi kumshukuru na kumsifu Yule alietuekea hali hiyo. Jambo hili hutekelezwa kwa kuonyesha utiifu wetu Kwake, kwa kujiepusha na kila aliyotukataza na kufanya kila aliyotuamrisha. Tutakapo tekeleza wajibu wetu wa utiifu kwa Mwenyezi Mungu, hapo tutakuwa tunatoa shukurani zetu kwa Baraka Zake, jambo ambalo litakalo kutusababishia kuzidi kubarikiwa kama alivyotuahidi Mwenyezi Mungu kutokana na Ne'ema Zake. Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) (kama ilivyo fasiriwa):

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

وَمَا بِكُم مِّن نِّعْمَةٍ فَمِنَ ٱللَّهِ

"Na neema yoyote mliyonayo, basi imetoka kwa Mwenyezi Mungu." [Soorah an-Nahl 16:53]

Na Akasema tena Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) (kama ilivyo fasiriwa):

وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ ﴿٧﴾

Na (Kumbukeni) alipotangaza Mola wenu (kuwa) "Kama mkishukuru, nitakuzidishieni; na kama mkikufuru, (jueni) kuwa adhabu Yangu ni kali sana." [Soorah Ibraaheem 14:7]

Enyi Waislamu:
Alhamdulillaah, sisi tunaishi katika ardhi hii tukiwa kwenye hali ya usalama na amani, lakini hali hii ya usalama na amani haiwezi kuendelea isipokuwa kwa kuwa na utiifu kwa Mwenyezi Mungu. Maadamu sisi bado tutaendelea kuamrisha mema na kukataza maovu, maadamu sisi bado tutaendelea kushirikiana katika kuamrisha mema na kukataza maovu, kwani wale wanaoamrisha mema na kukataza maovu ndio walio kwenye mstari wa mbele katika Ummah, na wao huzizuia sababu za kuadhibiwa na mateso, kwahivyo inatupasa kuwasaidia na kujiunga nao. Iwapo wao watakosea basi sisi tuwajulishe kuhusu makosa yao na tuwatahadharishe kuhusiana na makosa hayo na tuwaongoze kwenye uongofu na wala tusiyafanye makosa yao yakawa ndio sababu ya kuwaweka mbali na kuwatenga kutoka kwenye jukumu hilo - hiyo sio njia ya sawa...

Enyi Waislamu:
Misiba yoyote na maafa iliyowasibu watu katika mali zao au usalama wao, watu binafsi au katika jamii ni kutokana na madhambi yao na kuzipuuza Amri za Mwenyezi Mungu na sheria Zake alizotuteremshia, na kujitafutia Hukmu miongoni mwa watu zinazo pingana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu - aliewaumba viumbe wote na akawa na huruma nao kuliko mama zao na baba zao, na Yeye ndie ajuae zaidi kuliko nafsi zao kuhusu mambo yalio na manufaa nao.

Enyi Waislamu:
Mimi nayarudia tena maneno haya kwa sababu ya umuhimu wake na pia kwa sababu watu wengi huupa mgongo umuhimu huwo:
Mimi nasema: Misiba yoyote na maafa iliyowasibu watu katika mali zao au usalama wao, watu binafsi au katika jamii ni kutokana na madhambi yao na kuzipuuza Amri za Mwenyezi Mungu na sheria Zake alizotuteremshia, na kujitafutia Hukmu miongoni mwa watu zinazo pingana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu - aliewaumba viumbe wote na akawa na huruma nao kuliko mama zao na baba zao, na Yeye ndie ajuae zaidi kuliko nafsi zao kuhusu mambo yalio na manufaa nao.

Amesema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), katika kuyaeleza hayo kwenye Kitabu Chake, ili tuwe na mazingatio na kuwa na hadhari (kama ilivyo fasiriwa):

وَمَآ أَصَـٰبَكُم مِّن مُّصِيبَةٍ فَبِمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُواْ عَن كَثِيرٍ ﴿٣٠﴾

"Na misiba inayokupateni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu, na (juu ya hivi Mwenyezi Mungu) anasamehe mengi." [Soorah ash-Shoora 42:30]

Na Akasema Mwenyezi Mungu (kama ilivyo fasiriwa):

مَّآ أَصَابَكَ مِنْ حَسَنَةٍ فَمِنَ ٱللَّهِ ۖ وَمَآ أَصَابَكَ
مِن سَيِّئَةٍ فَمِن نَّفْسِكَ ۚ

"Wema uliokufikia umetoka kwa Mwenyezi Mungu; na ubaya uliokufikia umetoka nafsini mwako (Mwenyewe umefanya mambo hata yakakufika hayo)." [Soorah an-Nisaa' 4:79]

Mazuri yoyote tunayoyapata - Baraka na Usalama - yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, hayo yametokana na Yeye Peke Yake, mwanzoni mwake na mwisho, kutoka katika Rehma Zake. Ni Yeye alietupa sisi kutoka katika fadhila Zake yakwamba tunafanya yale yanayo sababisha kupatikana mambo yote tuyafanyayo, na ni Yeye anaetutilia Baraka Zake na kutukamilishia yote tunayoyafanya...

Ama kuhusu maovu yoyote yanayotusibu, iwapo ni njaa au khofu, au kitu chochote chenye kusababisha madhara, basi ni kwa ajili ya nafsi zetu wenyewe, sisi ndio tuliojidhulumu nafsi zetu na kujisababishia maangamivu.

Enyi Watu:
Watu wengi leo hudhania yakwamba misiba inayowafika, kama inahusiana na mali na matumizi ya fedha, au usalama na matukio ya kisiasa ni kwa ajili ya kitu halisi, sababu za kisiasa, sababu za umasikini, au matatizo yenye kusababishwa na mipaka. Hapana shaka yakwamba haya ni kulingana na kiwango chao cha ufahamu na udhaifu wa *Eamaan* zao na ukosefu wao wa kukizingatia Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume Wake (Sallallahu 'alayhi wasallam).

Enyi Waislamu, Wenye kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (Sallallahu 'alayhi wasallam): Nyuma ya sababu hizi kuna chanzo ambacho kimekwisha elezwa ukweli wake na Mwenyezi Mungu, sababu na chanzo cha mikasa hii iliyo na nguvu mno, mikubwa zaidi na yenye kuleta matokeo mabaya kuliko sababu za malimwengu. Hatahivyo sababu za malimwengu huwenda zikawa ndio sababu zenye kuleta yanayostahiki katika sababu zilizoandikwa na Mwenyezi Mungu ambazo ni zenye kulazimisha mikasa na adhabu. Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) (kama ilivyo fasiriwa):

ظَهَرَ ٱلْفَسَادُ فِى ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِى ٱلنَّاسِ لِيُذِيقَهُم بَعْضَ
ٱلَّذِى عَمِلُوا۟ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٤١﴾

"Uharibifu (madhambi na maasia kwa Mwenyezi Mungu n.k) umedhihiri barani na baharini kwa sababu ya yale iliyoyafanya mikono ya watu (dhulma, vitendo viovu n.k) ili Awaonjeshe (adhabu ya) baadhi ya mambo waliyoyafanya, hwenda wakarudi (wakatubia kwa Mwenyezi Mungu)." [Soorah ar-Room 30:41]

Enyi watu, Enyi Waislamu, Enyi Ummah wa Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam):
Mshukuruni Mwenyezi Mungu kwa Baraka Zake ambazo sasa hivi mumekurubia kuzisikia zikitajwa. Enyi Taifa la Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam) nyinyi ni wabora na mulio na heshima kubwa miongoni mwa mataifa ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah). Mwenyezi Mungu haliadhibu

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Taifa hili kutokana na maasia yake na madhambi wanayoyafanya kama alivyowaadhibu mataifa yaliopita. Hatoleta maangamivu ya adhabu ya kuwagharikisha kama ilivyotokea kwa kina 'Aad (Angalia Soorah al-Haaqqah 69:6-7), walipoangamizwa kwa kimbunga kikubwa Alipowafungulia kwa muda wa usiku wa siku saba na mchana wa siku nane kwa mfululizo ikawa wameanguka chini kama vigogo vya mtende - jee unawaona mabaki yao popote? Hatouangamiza Ummah huu mfano kama wa Thamood (Angalia Soorah al-Haaqqah 69:5) waliokabiliwa na ukelele utishao na mtetemeko wa ardhi hadi wakawa maiti zao wameinama mfano wa kusujudu katika majumba yao. Na Hatouangamiza kwa mfano wa watu wa loot (Angalia Soorah al-A'raaf 7:80-84), ambao Mwenyezi Mungu Aliwapelekea kimbunga kikali na mawe kutoka mbinguni na kuyapindua majumba yao juu chini.

Enyi Waislamu:
Ni katika Hikma na Rehma za Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), yakwamba Yeye huliadhibu taifa hili kutokana na madhambi na maasia walio nayo kwa kuyafanya baadhi yao kuwavamia baadhi nyengine ili waangamizane na washikane mateka wao kwa wao. Akasema Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) (kama ilivyo fasiriwa):


قُلْ هُوَ ٱلْقَادِرُ عَلَىٰٓ أَن يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّن فَوْقِكُمْ
أَوْ مِن تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ أَوْ يَلْبِسَكُمْ شِيَعًا وَيُذِيقَ بَعْضَكُم
بَأْسَ بَعْضٍ ۗ ٱنظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ ٱلْآيَٰتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُونَ ﴿٦٥﴾
وَكَذَّبَ بِهِۦ قَوْمُكَ وَهُوَ ٱلْحَقُّ ۚ قُل لَّسْتُ عَلَيْكُم بِوَكِيلٍ ﴿٦٦﴾ لِّكُلِّ نَبَإٍ
مُّسْتَقَرٌّ ۚ وَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾

"Sema: 'Yeye ndiye Mwezaji wa kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu, au kukuvurugenivurugeni (Muwe) makundi (yasiyopatana), na (Mweza wa) kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzao.' Tazama jinsi Tunavyoeleza Aayah (kwa namna hii) ili wapate kufahamu. (Nao hawataki kufahamu). Na watu wako (Ewe Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam)) wameikadhibisha (Qur'aan) hali hiyo ni haki. Sema: 'Mimi si mlinzi juu yenu'. Kila khabari (iliyotajwa hapa) ina wakati wake (maalumu kwa kufika). Na hivi karibuni mtajua (haya)." [Soorah al-An'aam 6:65-67]

Al-Haafidh Ibn Katheer akadondoa idadi ya Ahaadeeth katika Tafseer yake ya Aayah ya kwanza. Miongoni mwake ni ile iliyopokewa na Imaam al-Bukharee kutoka kwa Jaabir ibn 'Abdullaah (Radhiallahu 'anhu) aliesema:

"Pindi ilipoteremshwa Aya (ifuatayo) (kama ilivyo fasiriwa):

"Sema: 'Yeye ndiye Mwezaji wa kukuleteeni adhabu kutoka juu yenu..."

Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) akasema: 'Mimi najilinda kwa Uso wako'.

"...au kutoka chini ya miguu yenu..."

Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) akasema: 'Mimi najilinda kwa Uso wako'.

"au kukuvurugenivurugeni (Muwe) makundi (yasiyopatana), na (Mweza wa) kuwaonjesha baadhi yenu jeuri ya wenzao."

Mtume (Sallallahu 'alayhi wasallam) akasema: 'Hili ni jepesi' au '...sahali.'"

[Imepokewa na Imaam al-Bukharee katika Saheeh yake (Tarjimu ya Ki-ingereza vol. 6, uk.120-121 mlango wa 152)]

Ikapokewa na Imaam Muslim kutoka kwa Swahaba Sa'd ibn Abee Waqqaas (Radhiallahu 'anhu) aliesema: "Tulikwenda pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallahu 'alayhi wasallam) mpaka tukafika kwenye msikiti wa Banoo Mu'aawiyah, Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallahu 'alayhi wasallam) akaingia ndani ya msikiti huo na kuswali raka'ah mbili na sisi tukaswali nae. Baadae akamlingania Mola Wake kwa muda mrefu, kisha akasema: 'Nimemuomba Mola wangu mambo matatu: Nilimuomba asiliangamize Taifa langu kwa kuligharakisha Nae Akanikubalia hilo; Nikamuomba asiliangamiza Taifa langu kwa njaa - kama ilivyotokea kwa watu wa Fir'awn Nae Akanikubalia hilo; na nikamuomba yakwamba (Ummah wangu) wasiwe na ugomvi miongoni mwao - Lakini (Mola wangu) hakunikubalia hilo.'"

Katika Hadeeth iliyopokewa na Imaam Ahmad, an-Nasaa'ee na at-Tirmidhee, kutoka kwa Khabbaab ibn al-Aratt, (Radhiallahu 'anhu), aliesema: "Nilikwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallahu 'alayhi wasallam) katika usiku ambao nilimkuta akiswali kucha hadi alfajiri, na hatimae akamalizia swala yake kwa tasleem. Nikasema: 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu: Katika usiku wa leo nimekuona ukiswali jinsi ya swala ambayo sijawahi kukuonapo ukiiswali.' Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallahu 'alayhi wasallam): Kwa hakika hiyo ilikuwa ni swala ya matumaini na khofu. Ndani yake nilimuomba Mola wangu (Subhaanahu wata'aalah) mambo matatu, Nae Akanitakabalia mawili na kunikatalia moja. Nilimuomba Mola wangu, (Subhaanahu wata'aalah), yakwamba asituangamize sisi kwa yale aliyowaangamizia mataifa yaliokuja kabla yetu - Nae Akanitakabalia hilo; Nikamuomba Mola wangu, (Subhaanahu wata'aalah), yakwamba Asitudhalilishe kwa kutuletea adui asiekuwa miongoni mwetu - Nae Akanitakabalia hilo; na nikamuomba Mola wangu, (Subhaanahu wata'aalah), yakwamba asitusababishe sisi kugawanyika kwenye makundi tafauti, tukafanyiana uadui wenyewe kwa wenyewe, lakini Akanikatalia hilo.'"

Munaamini Aayaat hizi na munaamini riwaya zilizo saheeh kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallahu 'alayhi wasallam) basi ni kwanini musizizingatie? Kwanini musizizingatie?

Kwanini musizidhanie sababu hizi za misiba inayotokea kuwa ni kwa ajili ya udhaifu wenu wenyewe wa utekelezaji wa Dini ili muweze kurudi kwa Mola wenu mupate kuziokoa nafsi zenu kutokamana na yenye kusababisha kugharakishwa kwa maangamivu?

Kwahivyo mcheni Mwenyezi Mungu Enyi watumwa wa Mwenyezi Mungu na muziangalie hali zenu na mutubie mbele ya Mola wenu na muzirekebishe njia zenu zinazoelekea Kwake. Jueni, Enyi Taifa yakwamba adhabu hizi zinazowasibu na mikasa hii inayowakumba ni vitendo vyenu wenyewe na ni kwa ajili ya madhambi yenu. Basi kwa kila adhabu tubia na urudi kwa Mwenyezi Mungu na ujilinde Kwake (Subhaanahu wata'aalah), kutokamana na mitihani; mitihani ya kilimwengu inayohusiana na mtu: mauaji, madhara na kutolewa majumbani mwenu kwa nguvu; mitihani inayohusiana na mali: upungufu na ukosefu; na mitihani inayohusiana na Dini (muelekeo ulioekwa na Mwenyezi Mungu) - shaka na hawaa zinazochochea nyoyo na kuupoteza Ummah mbali na Dini ya Mwenyezi Mungu, na kuupoteza mbali na njia ya Watangulizi wetu wema (Salaf) na kuupeleka kwenye Maangamivu. Mitihani ya nyoyo ni miovu mno na ina fitina zaidi kuliko mitihani mengine yoyote ulimwenguni kwani mikasa ya kilimwengu inapotokea husababisha hasara ya hapa duniani tu, ambazo hazina budi kumalizika, ema hivi karibuni au baadae lakini mitihani inayohusiana na Dini husababisha hasara ya hapa ulimwenguni na kesho Aakhera: Maelezo haya yanapatikana katika Qur'aan (kama ilivyo fasiriwa):

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

قُلْ إِنَّ ٱلْخَـٰسِرِينَ ٱلَّذِينَ خَسِرُوٓاْ أَنفُسَهُمْ وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ ۗ
أَلَا ذَٰلِكَ هُوَ ٱلْخُسْرَانُ ٱلْمُبِينُ ﴿١٥﴾

"Sema (Ewe Muhammad (Sallallahu 'alayhi wasallam)): Hakika watakaopata hasara ni wale waliozitia hasarani nafsi zao na watu wao siku ya Kiama. Angalieni! Hiyo ndiyo hasara iliyo dhahiri." [Soorah az-Zumar 39:15]

Ewe Mwenyezi Mungu, tunakuomba tukiwa kwenye hali ya kuisubiri Ahadi Yako iliyo miongoni mwa wajibu uliotufaridhia sisi - Yakwamba utuja'alie sisi kuwa ni miongoni mwa wale wenye kuwaidhika na Alama Zako na kuyapokea maonyo pindi adhabu Yako inaposhuka.

Ewe Mwenyezi Mungu, Uja'alie Ummah wetu wa kiislamu na viongozi wake warudi Kwako kihakika kwa dhahiri na kwa siri, katika maneno yao na vitendo vyao ili Ummah huu upate kurekebishika, kwani kurekebishika kwa viongozi ndio sababu ya kurekebishika kwa Ummah.

Ewe Mwenyezi Mungu, tunakuomba uwaongoze wale walio na majukumu ya mambo ya Waislamu na Uwaja'alie wawe ni wenye kuyasikiliza na kuyashughulikia matukio ya Waislamu na uwaongoze kwenye kila Uyapendayo na yaliyo mazuri - Ewe Bwana wa Ulimwengu.

Ewe Mwenyezi Mungu, Tunakuomba uwaepushie kila mshauri alie fatani - Kwa hakika Wewe ni Muweza wa kila kitu.

Ewe Mwenyezi Mungu, Waongoze wao kupitia kwa washauri wema wanao-ongoza kwenye wema - wale watakaowapa naseeha na kuwahimiza kwenye wema - Ewe Bwana wa Ulimwengu.

Ewe Mwenyezi Mungu, yeyote miongoni mwa washauri wa wale walio na mamlaka juu ya Waislamu si washauri mwenye Ikhlasi kwao, wala kwa watu, Tunakuomba uwaondoe na utuletee walio bora kuliko wao - Ewe Bwana wa Ulimwengu, Ewe Mwenye Enzi na Utukufu.

Kila Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Bwana wa Ulimwengu, Tunakuomba uzifikilize Salamu juu ya Mtume wetu Muhammad, juu ya ahli zake, wafuasi wake wa kweli na maswahaba zake wote. Aameen.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Sehemu ya Pili

Kila aina ya Sifa njema ni zenye kumstahiki Mwenyezi Mungu, Sifa nyingi zilizo na Baraka na Utakaso kama Apendavyo Mola wetu na Anavyoridhia, na nashuhudia yakwamba hapana anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, PekeYake, asiekuwa na mshirika. Kila Sifa njema ni zake Yeye kuanzia mwanzo hadi mwisho. Nashuhudia yakwamba Muhammad ni mtumwa Wake na Mjumbe, ambae aliemchagua Yeye mwenyewe na akamfanya kuwa ni *Khaleel* Wake. Mwenyezi Mungu amuinue daraja yake na amfikilizie salamu, pamoja na ahli yake, maswahaba zake na wote waliofuata njia yake.

Mwanzo kabisa:

Ewe mtumwa wa Mwenyezi Mungu! Mche Mwenyezi Mungu, (Subhaanahu wata'aalah), na ujitahadhari na kuzidharau amri tulizoekewa na Mwenyezi Mungu... na ujitahadhari na kuzidharau Alama za Mwenyezi Mungu... na ujitahadhari na kuwacha kukitafakari Kitabu cha Mwenyezi Mungu... na ujitahadhari na kutojali kuzijua Sunnah za Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallahu 'alayhi wasallam) - kwani kufaulu ni kutokana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume wake (Sallallahu 'alayhi wasallam) (ukishikamana nazo, ukithibitisha ukweli wa ujumbe wake na kufuata amri zake) hapa ulimwenguni na kesho Aakhera.

Enyi watumwa wa Mwenyezi Mungu...
Kuna baadhi ya watu wenye shaka na kutafuta yanayo-sababisha mishkili yakwamba madhambi ndiyo yenye kusababisha misiba na taabu, na yakwamba hiyo ni kwa sababu ya udhaifu wa imani zao na kuwacha kukitafakari Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), na sasa nitawasomea kwa faida ya watu kama hao maneno ya Mwenyezi Mungu, (Subhaanahu wata'aalah), (kama ilivyofasiriwa):



"Na lau kama watu wa miji wangaliamini na kuogopa (kuwa na Taqwaa), kwa yakini tungaliwafungulia baraka za mbingu na ardhi. Lakini walikadhibisha (Mitume); tukawapatiliza (adhabu) kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma (ushirikina, ma'asia n.k). Je, watu wa miji (hii walio wabaya) wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafikia usiku, hali wamelala? Au watu wa miji (hiyo) wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafikia mchana, hali wanacheza? Je, wameaminisha kuadhibiwa na Mwenyezi Mungu? Hawaaminishi adhabu ya Mwenyezi Mungu ila watu ambao (watakuwa) wenye khasara." [Soorah al-A'raaf 7:96-99]

Mmoja miongoni mwa watu wema waliotutangulia (Salaf) alisema: "Ukimuona mtu akineemeshwa na Mwenyezi Mungu kwa kubarikiwa, na kisha mtu huyo akawa anaendelea kumu'asi Mwenyezi

Mungu, basi jua yakwamba hiyo ni kutokana na mipango ya Mwenyezi Mungu dhidi yake na kuwa mtu huyo ndie aliekusudiwa na Mwenyezi Mungu Aliposema katika Qur'aan (kama ilivyofasiriwa):

"Tutawavuta kidogo kidogo (waingie mikononi mwetu - adhabuni) kwa namna ambayo wenyewe hawajui (kuwa ndio kutiwa mkononi huko). Nami nitawapa muda (hao wabaya, sitawalipa upesi upesi). Hakika nguvu zangu ni madhubuti (baraabara). " [Soorah al-A'raaf 7:182-183]

Enyi Waislamu, Enyi wenye kumuabudu Mwenyezi Mungu:
Naapa kwa Jina La Mwenyezi Mungu (Wallaahi), madhambi yanasababisha kubadilika kwa usalama wa nchi; huibadilisha amani yake; huyabadilisha mafaniko yake; uchumi wake; na yanabadilisha nyoyo za watu wake. Madhambi husababisha fitina baina ya watu. Madhambi humsababisha Muislamu kumdhania nduguye Muislamu kuwa kama alie katika dini nyengine isiyokuwa Uislamu.

Lakini tukijitahidi kujirekebisha nafsi zetu, ahli zetu (familia zetu), majirani zetu na wale wanaoishi katika sehemu zetu, na kila tuwezae kumrekebisha, iwapo tutasaidiana kuhimizana mema na kukatazana maovu, iwapo tutawasaidia wenye kufanya hayo kwa hikma na mawaidha mema - basi italeta mazao ya umoja na mapenzi. Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) Akasema (kama ilivyofasiriwa):



"Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri (Uislamu) na wanaoamrisha mema na wakakataza maovu. Na hao ndio watakaotengenekewa. Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi (za kuwakataza hayo). Na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa." [Soorah Aali-'Imraan 3:104-105]

Najilingania nafsi yangu na kuwalingania nyote, Enyi ndugu zangu, tushikamaneni sote juu ya Dini ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah); tusaidianeni katika kuistawisha Sheria ya Mwenyezi Mungu; tuweni na ikhlaas tunapopeana naseeha kwa hikma na mawaidha mema; tujadilianeni na wale tunaostahiki kujadiliana nao kwa wema na kwa kuwatosheleza kwa ushahidi wa maandishi na ushahidi wa ki-akili na wala tusiwahame watu wapotofu juu ya upotofu wao kwani wao wana haki juu yetu yakwamba inatupasa sisi kuwaeleza ukweli na kuwahimiza waufuate na kwamba tuwaeleze huwo upotofu wao na kuwaonya wajitahadhari nao.

Lakini kuhusu kubakia kuwa taifa lenye kutengana na kila mmoja kipekee (asijali kumuhusu mwengine) na watu wakawa hawaoneani tena huruma basi yeyote asiejali kuwahusu Waislamu si miongoni mwao.

Enyi Waislamu, mimi nasema na narudia tena yakwamba tunawajibika, kama Waislamu na Waumini yakuwa tuyatizame kila yanayotokea na mikasa kulingana na ufahamu wenye busara wa ki-Islamu kama yalivyo-onyeshwa katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunnah za Mtume Wake (Sallallahu 'alayhi wasallam). Kwani tukiangalia kwa mtizamo wa mazingira ya kilimwengu basi makafiri wametuzidi na nguvu zao ni kubwa katika nadhari ya malimwengu na wametuwacha mbali sana na kututawala kwa hayo. Hatahivyo, tukiangalia kwa mtazamo wa ki-Islamu kulingana na njia ya

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Kitabu na Sunnah basi tutayatupilia mbali yote hayo tunayodhania kuwa ndiyo yaliyo sababisha misiba hiyo, na ikiwa tutarudi kwa Mwenyezi Mungu na kuinusuru Dini ya Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), basi Amesema Mwenyezi Mungu katika Kitabu chake, Nae ni Mkweli mno katika kueleza na Muweza Alie mtenza-nguvu (Subhaanahu wata'aalah) (kama ilivyofasiriwa):

وَلَيَنصُرَنَّ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَقَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾ ٱلَّذِينَ إِن مَّكَّنَّٰهُمْ
فِى ٱلْأَرْضِ أَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَمَرُوا۟ بِٱلْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا۟
عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۗ وَلِلَّهِ عَٰقِبَةُ ٱلْأُمُورِ ﴿٤١﴾

"Na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia dini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda. Wale (Viongozi wa ki-Islamu) ambao tukiwamakinisha, (tukiwaweka uzuri) katika ardhi (wao) husimamisha Sala na wakatoa Zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya. Na marejeo ya mambo (ya viumbe vyote) ni kwa Mwenyezi Mungu." [Soorah al-Hajj 22:40-41]

Wala hakusema "Wale ambao tukiwamakinisha, katika ardhi hustawisha viwanja vya madhambi, kufanya mambo ya upuzi na utovu wa haya" bali Alisema (kama ilivyofasiriwa):

"Wale (Viongozi wa ki-Islamu) ambao tukiwamakinisha, (tukiwaweka uzuri) katika ardhi (wao) husimamisha Sala na wakatoa Zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya. Na marejeo ya mambo (ya viumbe vyote) ni kwa Mwenyezi Mungu."

Hebu zingatia kwa makini, Ewe Ndugu Muislamu, vipi ambavyo Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) Alivyosema (kama ilivyofasiriwa):

"Na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia dini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda."

Aliitilia hima ahadi hii ya msaada kwa matamshi ya kutilia mkazo: kiapo chenye kufungamana na kitu, herufi *Laam* ya kutilia mkazo, na herufi *Noon* ya kutilia mkazo. Akazidi kuitilia tena mkazo kwa kusema (kama ilivyofasiriwa):

"Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda."

Kwani kwa Nguvu zake na Utukufu wake Huwasaidia wale awatakao, na hebu tafakari jinsi Alivyozimalizia Aayah hizo mbili (kama ilivyofasiriwa):

"Na marejeo ya mambo (ya viumbe vyote) ni kwa Mwenyezi Mungu."

Kwahivyo mtu anaweza kusema kutokana na fikra zake za kimakosa: "Sisi tutasaidiwa vipi na kupewa ushindi dhidi ya mataifa haya ya makafiri yalio na nguvu na uwezo mkubwa kutushinda." Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), ameshatuambia yakwamba mambo yote yako chini ya usimamizi wake Peke yake na yakwamba Yeye ni Muweza wa kila kitu. Sisi sote tunajua jinsi mitetemeko ya ardhi inavyoleta maafa - inapotokea pindi Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), anapoiamrisha itokee: (kama ilivyofasiriwa):

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَآ أَرَدْنَـٰهُ أَن نَّقُولَ لَهُۥ كُن فَيَكُونُ ﴿٤٠﴾

"Kauli yetu kwa kitu tunachokitaka (kiwe), ni kukiambia: 'Kuwa;' basi kinakuwa tu."
[Soorah an-Nahl 16:40]

Na punde si punde kukatokea gharka iso-kifani kwa muda mchache ambayo mfano wake hauwezi kulinganishwa na talifa lilo na nguvu linavyoweza kugharakisha.

Naapa kwa Jina la Mwenyezi Mungu (Wallaahi), lau kama sisi tutaisaidia kikweli Dini ya Mwenyezi Mungu kama inavyotupasa basi tutapewa ushindi juu ya kila adui katika ardhi, lakini kwa bahati mbaya wengi wetu tumekuwa ni mikiya ya maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui wa Mtume Wake (Sallallahu 'alayhi wasallam) - tukivishuhudia vitimbi vyao dhidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (Sallallahu 'alayhi wasallam) na kisha tukiwaiga wanavyofanya. Pengine hata kwenda kuishi katika miji yao na kujiumbua viwiliwili vyetu - vijana vyetu vya kiume na vya kike - kwenye miji hiyo ambayo hapana kisikiwacho isipokuwa makengele ya makanisa... ambamo hakusikilizwi hata miadhini... ambapo hata Allaah (Subhaanahu wata'aalah), humsikii kutajwa... na pasipo-onekana chochote isipokuwa kufanya mambo ya upuzi na utovu wa haya...

Kwahivyo tunamuomba Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah), Awageuze waliopotea miongoni mwa Umma huu na kuwarudisha kwenye uongofu, na Atufanye sote tuwe ni wenye kusaidiana na kuwa na ushirikiano katika kufanya mambo mema mpaka tuuregeshe Ummah huu katika hali yake ya fahari iliyopotea na ya utukufu. Kwa hakika Yeye ni Muweza wa hayo.

Ewe Mwenyezi Mungu tutakabalie (vitendo vyetu vizuri). Kwa hakika Wewe ni Mwenye kusikiya na Kujua kila kitu.

Ewe Mwenyezi Mungu tutakabalie (vitendo vyetu vizuri). Kwa hakika Wewe ni Mwenye kusikiya na Kujua kila kitu.

Ewe Mwenyezi Mungu tutakabalie (vitendo vyetu vizuri). Kwa hakika Wewe ni Mwenye kusikiya na Kujua kila kitu.

Ewe Mwenyezi Mungu. mtukuze Muhammad kwa wafuasi wake wa kweli kama Ulivyomtukuza Ibraaheem na ahli ya Ibraaheem. Kwa hakika Wewe ni Mtukufu unaestahiki Sifa zote njema.

Ewe Mwenyezi Mungu, Mbariki Muhammad na Uwabariki wafuasi wa kweli wa Muhammad kama Ulivyombariki Ibraaheem na ahli ya Ibraaheem. Kwa hakika Wewe ni Mtukufu unaestahiki kila aina ya Sifa njema.